# GREAT START TO Quality

Supporting Excellence in Early Education

KUZINDUA
02.01.2023

## GSQ Inaanzisha Mfumo wa Utambuzi na Kuimarisha Ubora Uliokuzwa



KUTAMBULISHA

# Mchakato wa Uimarishaji Endelevu

Baada ya kushirikiana na watoa huduma na familia zinazotumia Great Start to Quality, tunaanzisha mchakato mpya kulingana na kilicho muhimu zaidi kwao: kuimarisha ubora katika mazingira ya malezi ya watoto ili watoto wajifunze na kustawi.

Ufadhili kutoka kwenye Ofisi ya Great Start ndani ya Idara ya Elimu ya Michigan unasaidia utekelezaji wa Great Start to Quality.

# Je, Ratiba Zinazotarajiwa za Masahihisho ya Great Start to Quality ni gani?

**Idara ya Elimu ya Michigan - Ofisi ya Great Start itaanzisha mchakato uliosahihishwa tarehe 1 Februari, 2023.**

2018
**Utafiti wa Uthibitishaji Ulikamilika**

2019
**Kamati ya Ushauri Kukutana**

2020
**Maoni Kutoka kwenye Makundi Changanuzi**

2021
**Kiashiria na Jaribio la CLASS**

2021
**Masahihisho kwenye Viashiria**

2022
**Uundaji wa Nyaraka za Mwongozo na Mawasiliano**

2023
**Uzinduzi Februari**

## Ni Nini Kinachofuata?

Chapa ya Great Start to Quality iliyobuniwa upya inazinduliwa kwa wabia na familia. Kutoka Mpango, Maono na Maadili yetu, hadi nembo, rangi na mchakato wetu mpya, tunayo furaha ya kusonga mbele katika maisha ya baadaye.

Tutawasiliana na familia za Michigan kwa kampeni ili kutangaza mabadiliko, kuzitambulisha kwa GSQ na kuzisaidia kuelewa faida tunazotoa ili kuzisaidia kupata watoa huduma wa ubora wa juu wa kuwasaidia watoto wao kustawi.

**Mfumo Endelevu wa Utambuzi na Kuimarisha Ubora**

## Hatua za Kutayarisha

- **Endelea Kuunganishwa – tembelea tovuti yetu, jisajili kwa jarida, fuata GSQ na Vituo vya Huduma kwenye Facebook.**
- **Unda wasifu wa mpango wa shirika katika MiRegistry**
- **Wafanyakazi wa mpango waliunda uanachama kupitia MiRegistry**
- **Jiunge kwenye Vituo vya Huduma**
- **Angalia MiRegistry kwa ajili ya mafunzo**
- **Kagua Viashiria vipya vya Ubora greatstarttoquality.org/reflecting-on-quality**
- **Kusanya nyaraka**
- **Jisajili kwa Mafunzo ya CLASS, ERS, SEL PQA**

Ufadhili kutoka kwenye Ofisi ya Great Start ndani ya Idara ya Elimu ya Michigan unasaidia utekelezaji wa Great Start to Quality.

## Mwishowe, Ni Nini Kimesalia Sawa na Mfumo wa Zamani?

Mipango ambayo ingependa kuchapisha kwenye Kiwango cha Kuonyesha Ubora itaendelea kukamilisha Uthibitishaji na Uangalizi katika Eneo utakaokamilika ndani ya siku 90 kutoka mwanzo wa mchakato wa uthibitishaji.

Vituo vya Huduma za Karibu vitapatikana kwa usaidizi wa kiufundi, mafunzo na ushauri kwa mipango na watoa huduma wanaohitaji. Viwango vyote vya ubora vilivyochapishwa vitatumika kwa miaka 2 na matokeo yatachapishwa kwa ajili ya familia kwenye wasifu wa mpango wa umma. Mipango inayoshiriki lazima iwe na ripoti nzuri ya utoaji leseni na iwe na hali ya utoaji leseni ya Asili, Kawaida, au ya Muda ya Kwanza. Mipango iliyochapisha ukadiriaji bado itastahiki nyongeza ya viwango vya fidia ya ruzuku.



## SAWA

- **Hupima ubora**
- **Uthibitishaji na Uangalizi katika Eneo**
- **Mchakato unachukua chini ya siku 90**
- **Usaidizi wa kiufundi, kufunza na ushauri unaotolewa na Vituo vya Huduma**
- **Matokeo yanayochapishwa kwa ajili ya familia kwenye wasifu wa mpango wa umma**
- **Tarehe ya mwisho ya miaka miwili**
- **Muunganisho wa ruzuku**
- **Lazima uwe katika hali hizi za utoaji leseni: Asili, Kawaida au ya Muda ya Kwanza**

## TOFAUTI

- **Lenga kuimarisha ubora badala ya ukadiriaji**
- **Kujitathmini kuhusu Viashiria vya Ubora**
- **CLASS, ERS na SEL PQA (Mipango ya OST Pekee) kwa Uangalizi katika Eneo**
- **Kila mpango unapitia mchakato sawa**
- **Mpango wa Kuimarisha Ubora unaooana na falsafa ya mpango**

Ufadhili kutoka kwenye Ofisi ya Great Start ndani ya Idara ya Elimu ya Michigan unasaidia utekelezaji wa Great Start to Quality.

Mpango, Maono na Maadili yetu ya chapa mpya yanatumika kama msingi wa Great Start to Quality tunaposonga mbele. Taarifa ya Mpango wetu inawakilisha sisi na sababu ya uwepo wetu. Maono yetu yanawakilisha pale tunapotaka kuwa siku zijazo. Maadili yetu yanawakilisha imani zinazoongoza ambazo zinachochea miunganisho ya sera ya ndani na ya nje ya chapa yetu kila siku.

## Mpango

Tunalenga hali za kujifunza mapema za ubora wa juu zinazojenga msingi kwa ajili ya stadi ambazo watoto wanahitaji ili kustawi katika shule na maisha.

Ili kufanikisha hili, tunatoa usaidizi wa kuimarisha watoa huduma wa Michigan wa malezi na elimu ya mapema ili waendelee kuimarisha huduma na usaidizi wanaowapa watoto wachanga, familia zao na jamii.



## Maono

Familia zote katika jimbo la Michigan zina uwezo wa kupata hali za mafunzo ya mapema ambazo ni salama na za ubora wa juu zinazowapa watoto msingi thabiti wa kustawi na kukidhi mahitaji yao wanapokua na kujifunza.

## Maadili

**USAWA**

Tunaamini katika ufikiaji wa usawa wa malezi na elimu ya mapema kwa familia zote zilizo Michigan. Tunashirikiana na wabia wa jimbo na jamii ili kuongeza idadi ya mipango kwenye jimbo zima na kuwahimiza watoa huduma kuendelea kuongeza ubora wao ili kuzisaidia familia na jamii.

**UBORA**

Tunaamini kwamba uimarishaji endelevu wa ubora wa mipango ya malezi na elimu ya mapema, kupitia maendeleo ya taaluma na kuangazia desturi za mpango, husaidia watoa huduma kutoa malezi ya ubora wa juu unaokidhi mahitaji ya familia na husaidia watoto kustawi.

**KUWEZESHA**

Tunaziwezesha familia kuwa watetezi wa watoto wao na kuelewa faida za malezi na elimu ya mapema ya ubora wa juu.
Tunawawezesha watoa huduma kuimarisha ubora kwa kujenga mahusiano thabiti ya kuaminika na kutoa taarifa, huduma na usaidizi mwingine ili kuimarisha ubora.

**KUJITOLEA**

Tumejitolea kuinua wataalamu wa malezi na elimu ya mapema na kusaidia wafanyakazi kupitia maendeleo ya taaluma na usaidizi wa elimu hali inayoongeza ubora wa malezi ambayo watoto wa Michigan hupokea.

Ufadhili kutoka kwenye Ofisi ya Great Start ndani ya Idara ya Elimu ya Michigan unasaidia utekelezaji wa Great Start to Quality.

## Je, Great Start to Quality ni Nini?

Great Start to Quality hutathmini ubora wa mipango ya malezi ya watoto na watoa huduma katika jimbo la Michigan. GSQ ni Mfumo wa Ukadiriaji na Kuimarisha Ubora wa Michigan (QRIS). Mtindo wa sasa unasaidia mipango ya huduma ya malezi ya watoto yenye leseni, chekechea na Out-of-School Time (OST) Pekee kwa ukadiriaji na uimarishaji ubora.

Viashiria vya Ubora ni viwango vinavyotumika kupima ubora wa mpango katika sehemu muhusus. GSQ hujitahidi kuzisaidia familia kufanya maamuzi bora kuhusu malezi ya watoto na kusaidia mipango ya malezi ya watoto kwa kuwa inaimarisha ubora wao na kutoa malezi bora yanayowezekana kwa watoto.

GREAT START TO Quality



## Je, Kwa Nini GSQ Inaimarishwa?

Lengo la sasa kuhusu ukadiriaji linawaacha watoa huduma wakihisi kama "wanaokagua kisanduku" ili kufanikisha ukadiriaji wa juu, badala ya kulenga mengi wanayoweza kuhusu uimarishaji wa ubora wa kweli. Kwa miaka mingi, watoa huduma wameshiriki jinsi muunganisho baina ya ukadiriaji wa nyota na mifumo mingine ya ukadiriaji (Yelp, Google, n.k.) huzipa familia muktadha usio sahihi wa kupima ubora wa mpango.

Pia tulipokea maoni kuhusu uteuzi mdogo wa mtaala, tathmini na zana za uchunguzi zilizoidhinishwa kwa malezi ya watoto ya nyumbani na watoto wachanga na watoto wanaodema. Mbinu na viwango vyetu kulingana na utafiti vitawafahamisha vizuri watoa huduma na familia kuhusu kuimarisha ubora kwa jumla.

## GSQ Inasasisha Mfumo Ili Kukuza Ubora na Usawa

Kulingana na mchango na mwongozo kutoka kwa wataalamu wa maudhui, washiriki watoa huduma, maoni kutoka kwa familia na jamii na Kamati ya Ushauri ya wadau tunaimarisha mfumo wa Great Start to Quality kuwa Mchakato Endelevu wa Kuimarisha Ubora.



Ufadhili kutoka kwenye Ofisi ya Great Start ndani ya Idara ya Elimu ya Michigan unasaidia utekelezaji wa Great Start to Quality.

# Uangalizi katika Eneo - Machaguo Zaidi

Great Start to Quality itatoa zana tatu tofauti za Uangalizi katika Eneo hivi karibuni. Machaguo yote yanaoana na mitindo ya taifa na hutumiwa sana kutathmini ubora wa mpango.

Classroom Assessment Scoring System (CLASS) na Environment Rating Scales (ERS) yatakuwa machaguo kwa mipango yenye watoto wachanga, watoto wanaodema na watoto wa chekechea.
Mipango ya kituo chenye Mipango ya Great Start Readiness na Head Start itatumia CLASS pekee.

Yote miwili husaidia aina mbalimbali za mitaala na falsafa za mipango. Zana ya Uangalizi katika Eneo, Social Emotional Learning Program Quality Assessment (SEL PQA), itatumiwa tu kwa madarasa na mipango ya Out-of-School Time (OST).



| Aina ya Mpango na Umri Unaohudumiwa | CLASS | ERS | SEL PQA |
|---|---|---|---|
| **Malezi ya Nyumbani** – Umri Unaohudumiwa 0-12 | X | X | |
| **Malezi ya Nyumbani** – Umri Unaohudumiwa 5-12 | | | X |
| **Malezi ya Nyumbani** – Ya Head Start ya Mapema | X | X | |
| **Kituo cha Malezi ya Watoto** – Umri Unaohudumiwa 0-12 | X | X | X |
| **Kituo cha Malezi ya Watoto** – Umri Unaohudumiwa 5-12 | | | X |
| **Kituo cha Malezi ya Watoto** – Cha Madarasa ya GSRP au Head Start | X | | |

Ufadhili kutoka kwenye Ofisi ya Great Start ndani ya Idara ya Elimu ya Michigan unasaidia utekelezaji wa Great Start to Quality.




## Kuangazia Ubora

Seti mpya ya Viashiria vya Ubora imeanzishwa. Mipango inayotimiza kiwango hiki cha ubora lazima itumie Viashiria vilivyosahihishwa vya Ubora katika Kujitathmini ili kuangazia uwezo wa mpango na kutambua malengo ya uboreshaji endelevu.

## Kukuza Ubora

Mipango inayotimiza kiwango hiki cha ubora lazima ikamilishe angalau lengo moja (1) katika Mpango wa Kuimarisha Ubora pamoja na tarehe ya mwisho. Lengo linaweza kutegemea Kujitathmini, Uangalizi katika Eneo, au huenda lisihusiane na GSQ.

## Kukuza Ubora-Kumethibitishwa

Mipango inayotimiza kiwango hiki cha ubora lazima ikamilishe angalau lengo moja (1), iwasilishe hatua ya Kujitathmini na kukamilisha mchakato wa Uthibitishaji. Mipango inaweza kusubiri kupokea Uangalizi katika Eneo.

## Kudhihirisha Ubora

Mipango inayotimiza kiwango hiki cha ubora lazima ikamilishe Uthibitishaji na alama za vigezo kwa ajili ya Uangalizi katika Eneo.

Ufadhili kutoka kwenye Ofisi ya Great Start ndani ya Idara ya Elimu ya Michigan unasaidia utekelezaji wa Great Start to Quality.



## Kuimarisha Ubora

- Masasisho kwenye Viashiria vya Ubora
- Orodha pana ya mtaala
- Usaidizi bora kwa falsafa za mipango mbalimbali
- Kulenga kuangazia kunakoelekezwa na mtoa huduma ili kufanya mabadiliko na kuunda mpango
- Watoa huduma wote waliopewa leseni walio na historia nzuri ya utoaji leseni ni sehemu ya GSQ
- Machaguo mapya ya zana ya Uangalizi katika Eneo: CLASS®, ERS na SEL PQA
- Nyota zitabadilishwa na viwango na kila mpango unafuata mchakato sawa

## Marekebisho ya Upendeleo

- Kubadilisha zana za Uangalizi katika Eneo ili kusaidia zaidi aina zote za mipango
- Kuangazia kiwango cha lugha na kusoma kulingana na maoni ya watoa huduma
- Kutoa huduma ya tafsiri na ukalimani katika mchakato mzima wa ukadiriaji
- Kurahisisha michakato ya mfumo
- Viashiria vya Ubora havikadiriwi kwa alama





Mtindo mpya unalenga kuimarisha ubora kama mchakato au safari endelevu. Ili kutoa malezi bora, lazima tutumie utafiti wa hivi punde na kuendelea kujifunza kuhusu na kukuza ubora wa mpango ili kuhudumia watoto na familia zetu vizuri.

Ufadhili kutoka kwenye Ofisi ya Great Start ndani ya Idara ya Elimu ya Michigan unasaidia utekelezaji wa Great Start to Quality.

## Ufanisi Huanza Kwa Huduma na Usaidizi wa Mafunzo Uliokuzwa Kwa Wafanyakazi Na Watoa Huduma

GSQ imejitolea kuhakikisha uimarishaji wa ubora kwa wote – kuendelea kutoa usaidizi na kuwafunza wafanyakazi na watoa huduma. Great Start to Quality ina Vituo vya Huduma katika kila eneo. Wafanyakazi hawa wa Vituo vya Huduma na Kuimarisha Ubora ni sehemu muhimu ya mfumo wa Great Start to Quality wanaoongoza na kuwasaidia watoa huduma kwa viwango vyote vya mafunzo yao ya taaluma na mipango endelevu ya uimarishaji.





## Je, Ni Nini Kilichobadilika Katika Mchakato Mpya?

Great Start to Quality itahamia katika mchakato wa Utambuzi na Kuimarisha Ubora – ulio na Viwango vya Ubora badala ya ukadiriaji wa nyota. Mtindo uliosahihishwa una machaguo zaidi na uwezo wa kubadilika wa mipango ili kuimarisha.

## Mabadiliko ya Lugha

Katika mchakato uliosahihishwa wa Great Start to Quality, mipango itatambua mabadiliko katika lugha inayotumiwa kwa sasa.

| Lugha ya Sasa | Lugha Iliyosahihishwa |
|---|---|
| • Mfumo wa Ukadiriaji na Kuimarisha Ubora | • Mfumo wa Utambuzi na Kuimarisha Ubora |
| • Mambo ya Kuangaziwa | • Malengo |
| • Utafiti wa Kujitathmini | • Kujitathmini |
| • Ukadiriaji wa Nyota | • Kiwango cha Ubora |
| • Tathmini katika Eneo | • Uangalizi katika Eneo |
| • Mshauri wa Kuimarisha Ubora | • Mkufunzi wa Kuimarisha Ubora |

Ufadhili kutoka kwenye Ofisi ya Great Start ndani ya Idara ya Elimu ya Michigan unasaidia utekelezaji wa Great Start to Quality.





- Mfumo wa Kukadiria na Kuimarisha Ubora utabadilika hadi **Mfumo wa Utambuzi na Kuimarisha Ubora**; mabadiliko haya yanatekelezwa ili **kuakisi kazi ambayo** mipango hukamilisha katika mchakato mzima wa kupokea Kiwango cha Ubora.
- Katika Mpango wa sasa wa Kuimarisha Ubora msemo Mambo ya Kuangaziwa unatumika. Katika mchakato wa **Great Start to Quality**, tutakuwa tukiita Mambo ya Kuangaziwa malengo.
- Mpango wa Self-Assessment Survey uliokamilishwa kwa sasa kwa ajili ya Uthibitishaji sasa utaitwa **Self-Reflection**; mabadiliko haya yanafanywa kuwa mpango unapaswa kuangazia desturi za mpango za sasa ili kutambua sehemu za uimarishaji.
- Mchakato wa sasa wa Tathmini katika Eneo utaitwa **Uangalizi katika Eneo** ili kuoana na mabadiliko katika zana zinazotumiwa katika mchakato uliosahihishwa wa Great Start to Quality.
- Mipango inatumiwa kwa sasa na Washauri wa Kuimarisha Ubora. Katika mchakato uliosahihishwa wa Great Start to Quality, cheo chao kitabadilika na kuwa **Mkufunzi wa Kuimarisha Ubora**.

Ufadhili kutoka kwenye Ofisi ya Great Start ndani ya Idara ya Elimu ya Michigan unasaidia utekelezaji wa Great Start to Quality.

GSQ

greatstarttoquality.org